**TANGAZO**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

## BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

Katibu Mtendaji, Baraza la Mitihani la Tanzania anapenda kuwajulisha watu wote wanaotarajia kufanya Mtihani wa **Kidato cha Sita** (**ACSEE**) mwezi **Mei 2027** kama Watahiniwa wa Kujitegemea kwamba;

1. Kipindi cha kawaida cha usajili wa Watahiniwa wa Kujitegemea kitakuwa kuanzia tarehe **01 Julai** hadi **30 Septemba, 2026** kwa ada ya Shilingi **50,000/=**. Aidha, watakaojisajili kwa **kuchelewa** yaani kuanzia tarehe **01 Oktoba** hadi **31 Oktoba, 2026** watalipa Shilingi **65,000/=** na hakutakuwa na usajili mwingine baada ya tarehe **31 Oktoba 2026**.

2. Usajili utafanyika kwa njia ya mtandao **(online)**. Aidha, kabla ya kujisajili, waombaji wanapaswa kwenda kwenye Vituo vya Mitihani kuchukua **Namba Rejea** (**Reference Number**) zinazotolewa **bure na** kufanya malipo ya ada kupitia Benki kwa kutumia ‘Control Number’.

3. Ufafanuzi kuhusu utaratibu na hatua za kufuata katika kutengeneza ‘**Control Number**’ na kujisajili, umetolewa katika tovuti ya Baraza la Mitihani la Tanzania: **www.necta.go.tz.** na kwa Wakuu wa Vituo vya Watahiniwa wa Kujitegemea

4. Waombaji wote **wanasisitizwa** kuhakikisha wanajisajili mapema kwani mfumo wa usajili utafungwa baada ya kipindi cha usajili kukamilika.

Imetolewa na;

**KATIBU MTENDAJI**